Kwa Nini Umkiri Yesu Kristo Mbele Za Watu?

na

Ellis P. Forsman

Kwa Nini Umkiri Yesu Kristo Mbele Za Watu?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Kwa Nini Umkiri Yesu Kristo Mbele Za Watu?

1 Tim. 6:11-16

1 Tim. 6:12-13, "*Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi. Nakuagiza mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele za Pontio Pilato.*"

Kifungu kimeeleza:

"*Maungamo mazuri.*"

Kwa nini hii inaitwa "*Maungamo mazuri*" mara mbili katika kifungu hiki kifupi?

Kwa sababu Kristo alilifanya chini ya kiapo (kwa liwali kabla hajapelekwa kwa Pilato).

Marko 14: 60-62, "*Kisha Kuhani Mkuu akasimama katikati, akamwuliza Yesu, akisema, Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini? Lakini akanyamaza, wala hakujibu neno. Kuhani Mkuu akamwuliza tena, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu? Yesu akasema, Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni.*"

Kwa sababu Mungu mwenyewe alilifanya mara mbili:

- **Wakati wa kubatizwa kwa Yesu,** Math. 3:17, "*Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*"
- **Wakati wa kudhiirishwa**, Math. 17: 5, "*Alipokuwa katika kusema, tazama wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.*"

Kwa sababu ni sehemu muhimu katika wokovu.

Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako yakuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa mayo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

Umuhimu wa swali,
“Kwa nini umkiri Yesu mbele za watu?”

Katika kifungu hiki cha maandiko inaunganishwa na “kujiweka katika uzima wa milele.”

Ni muhimu kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu ili kupata uzima wa milele. 1 Yohana 5:13, “*Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini jina la Mwana wa Mungu.*”

Maswali muhimu yanaulizwa kuhusu Yesu, yanaulizwa na Yesu:

- Math. 22:42, “*… Mwaonaje katika habari ya Kristo? Ni Mwana wa nani?...”*
- Math. 16:13, “*… Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?*”
- Math. 16:15, “*Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?*”

Katika nchi ya (Marekani) ambapo kuna Biblia katika kila mkono, ambapo watu wote kwa kiwango Fulani wanajua changamoto ya Kristo, swala la “Maungamo Mazuri” haliwezi kutathiminiwa. Karibia kila mtu katika nchi hii anajua kuhusu Yesu Kristo. Wengi wanakana kwamba ni Mwana wa Mungu, wanadai kwamba alikuwa tu ni nabii mzuri. Je wewe unasema kuwa alikuwa ni nani? Unaamini nini? Je ni Mwana wa Mungu? Jibu la swali hili ni muhimu kwa Mungu.

Ushahidi kwamba Yesu ni “Mwana wa Mungu”, “Masihi” aliyeahidiwa:

Simoni Petro aliutamka.

Math. 16: 15-19, “*Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simoni Petro akajibu akasema, <u>Wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai</u>. Yesu akajibu akamwambia, Heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni, na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*”

Malaika wa Mungu wanautamka:

Kwa Yusufu. Math. 1:18-23, "*Kuzaliwa kwake Yesu kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye Yusufu mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumuacha kwa siri. Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema Yusufu, mwana wa Daudi usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao. Hayo yote yamekuwa ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii ikisema. Tazama bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana ; nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani Mungu pamoja nasi.*"

Kwa Mariamu. Luka 1: 26-33, "*Mwezi wa sita Malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Mariamu. Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu, uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe. Naye akafadhaika sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani? Malaika akamwambia, usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama utachukua mimba na kuzaa mototo mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu ataitwa mwana wa aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho.*"

Yohana Mbatizaji alilitamka.

Yohana 1: 29-34, **"***Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, tazama, Mwana kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye niliye nena habari zake kwamba, yuaja mtu nyuma yangu ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. Wala mimi sikumjua; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nabatiza kwa maji. Tena Yohana akashuhudia akisema, Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni, naye akakaa juu yake. Wala mimi sikumjua lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu. Nami nimeona, tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu.*"

Nathanaeli alilitamka.

Yohana 1:47-51, "*Basi Yesu akamwona Nathanaeli anakuja kwake, akanena habari zake, tazama Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake. Nathanaeli akamwambia, umepataje kunitambua? Yesu akajibu akamwambia, kabla Filipo hajakuita ulipokuwapo chini ya mtini nilikuona. Nathanaeli akamjibu, Rabi, wewe u Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israeli. Yesu akajibu akamwambia, kwa sababu nilikuambia, nilikuona chini ya mtini, waamini? Utaona mambo makubwa kuliko haya. Akamwambia, Amin, amin nawaambia mtaziona mbingu zimefunguka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya Mwana wa Adamu.*"

Nikodemo alilitamka.

Yohana 3:1-2, "*Basi palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi. Huyo alimjia usiku, akamwambia Rabi twajua ya kuwa u mwalimu umetoka kwa Mungu kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye."* Yesu akaongea naye, Yohana 3:14-16, "*Na kama vile Musa alivyomwinua Yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Towashi wa Kushi aliamini na akalitamka.

Matendo 8:26-38, "*Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa. Naye akaondoka akaenda mara akamwona mtu wa Kushi, towashi mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea ameketi garini mwake akisoma chuo cha Nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo, sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia akisoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je! Yamekuelea haya unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili,aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule towashi akamjibu Filipo, akasema, nakuomba, nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake,*

naye akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, yazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe [Filipo akasema, ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.] Akaamuru lile gari lisimame wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza."

Kwa nini ufanye ungamo zuri?

Ni mwamba ambalo kanisa linajengwa juu yake.

Math. 16:15-19, "*Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, Heri wewe Simoni Baryona kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbingu. Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Name nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*"

Inatuletea ujuzi wa Kristo.

Math. 10:32, "*Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni.*"

Ni katika wokovu.

Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

Imani kabla ya kukiri alafu ubatizo.

Matendo 8:37-38, "*Filipo akasema, ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu akanena, naamini ya kuwa Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame, wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi naye akambatiza.*"

Wuongofu zingine:

Wasamaria na Simoni mchawi, Matendo 8:12-13, "*Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo wakabatizwa, wanaume na wanawake. Na yeye*

Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa akashikamana na Filipo; akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka."

Kornelio na nyumba yake (Mataifa), Matendo 10:47-48, "*Ni nani awezaye kuzuia maji hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha.*"

Lidia na nyumba yake, Matendo 16:14-15, "*Mwanamke mmoja jina lake Lidia mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo. Hata alipokwisha kubatizwa yeye na nyumba yake akatusihi akisema, kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa Bwana, ingieni nyumbani mwangu mkakae. Akatushurutisha.*"

Sauli wa Tariso (Paulo), Matendo 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*"

Tukiyaweka yote pamoja

Katika mifano inayoendelea na picha zingine, tunaona mpango wa Mungu wa wokovu. Ni kawaida kwamba imani, toba, kukiri, na ubatizo ziliitajika na Mungu kwa ajili ya uongofu wa mwenye dhambi. Hii mifano, kila mmoja haionyeshi kila mfumo wa uongofu; lakini hitimisho ni kawaida. Ukweli kwamba kila hatua ya mfano haikuonyeshwa, tunajua kutoka katika maandiko mengine kwamba inatokea. Mungu hawezi kusema uongo.

Uwazi na vitendo vya kuacha zimetokea kwenye maandiko, siyo kwamba havikutokea, lakini kwa sababu mwandishi ameonyesha tu sehemu ya mlolongo wote.

Katika Matendo 8:38 ni dhahiri kwamba walikuwa na "imani" sehemu zingine wasingeweza kuuliza maswali, "tutendeje ndugu zetu?" baada ya kusikia injili imehubiriwa.

Je inaleta maana kudhania kwamba katika kila uongofu waliruhusiwa kufanya chochote ambacho walitaka kufanya? Wengine wanaamini pekee (wengine leo wanaamini hivyo)? Wengine huamini na kutubu? Wengine wanaamini, wanatubu, na wanabatizwa? Wengine huamini, wanatubu, wanakiri, bila kubatizwa? Hakika, ubatizo unaonyeshwa zaidi ya mfumo mwingine wowote wa uongofu.

Hitimisho

Imani, Roba, na Kukiri huongoza mtu KWA Kristo, lakini ni Ubatizo ndiyo unamuweka mtu KATIKA Kristo.

- Waru. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"
- Wagal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Baada ya uongofu kwa Yesu Kristo, kukiri kwetu kwa Yesu hakuishi. Ni wajibu wa kila Mkristo kupeleka jina la Kristo kwa ulimwengu. Marko 16: 15, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe.*"

Hebu na tusiache wokovu ambao umewekwa mbele yetu. Waeb. 2:3, "*sisi je! Tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitishwa kwetu na wale waliosikia.*"

Kwa nini usifanye ungamo zuri hilo leo? Watu wote baadaye watalifanya.

Wafil. 2:9-11, "*Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.*"

Kwa nini usifanye sasa?

-